JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## KUZINGATIA HITAJI LA KISHERIA LA KUSAJILI NA KUTUMIA MAJINA YA DOT TZ (.TZ DOMAIN NAMES) NCHINI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 79 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Cap. 172 R.E. 2023, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina wajibu wa kusimamia uendeshaji wa rajisi ya majina ya vikoa vya .tz (.tz domain names registry) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kanuni ya 3(1) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Usimamizi wa Majina ya Vikoa) 2020, iliyorekebishwa mwaka 2023, inazitaka kampuni, taasisi za serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, ubia, au mashirika ya kijamii yaliyosajiliwa na kufanya biashara nchini Tanzania ambayo yanafanya mawasiliano kwenye mtandao wa intaneti, kusajili na kutumia majina ya kikoa cha dot tz.

Vilevile, Kanuni ya 3(2) inataka jina la kikoa lililosajiliwa litumike kwa mawasiliano yote rasmi ya kielektroniki isipokuwa kama imethibitishwa kitaalamu kuwa haiwezekani. Pia, Kanuni ya 25 inatamka kwamba mtu yeyote mwenye jina la kikoa ambalo halizingatii Kanuni iliyotajwa hapo juu atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

**Kwa muktadha huu, TCRA** inazikumbusha kampuni, taasisi za serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na kijamii yaliyosajiliwa na kufanya shughuli nchini, kutekeleza matakwa ya kisheria yaliyotajwa hapo juu kwa kusajili na kutumia majina ya vikoa vya dot tz.

Usajili wa majina ya dot tz (.tz) unaweza kufanywa kwa kutembelea **https://karibu.tz**. Kwa maelezo zaidi kuhusu usajili huo na masuala mengine yanayohusiana nayo, tafadhali wasiliana na TCRA kupitia anuani iliyopo hapa chini.

Imetolewa tarehe **29 Julai 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Tue Jul 29 20:54:37 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz